

HALMASHAURI YA MANISPAA KIGOMA/UJIJI

SHULE YA SEKONDARI BUZEBAZEBA,
S. L. P. 44,
KIGOMA.

Kumb. Na. MLS/F.7/II/19

Tarehe:

JINA LA MWANAFUNZI
S. L. P.
.....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI BUZEBAZEBA, MWAKA 2021.

1.0 UTANGULIZI

Nafurahi kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na Kidato cha kwanza mwaka 2021 katika Shule hii. Shule ya Sekondari Buzebazeba ni ya kutwa na iko katika Kata ya Buzebazeba, umbali wa kilometra moja (01) tu, upande wa mashariki kutoka Ofisi ya Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji.

Muhula wa kwanza wa masomo siku ya Jumatatu, tarehe 11/01/2021 saa 1.30 asubuhi kwa hiyo unatakiwa kuripoti shulenii mapema siku hiyo bila kuchelewa.

Mwisho wa kuripoti shulenii itakuwa tarehe 25/01/2021, baada ya hapo mwanafunzi hatapokelewa shulenii.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

2.1. Sare za Shule

a. Wavulana

- i. Shati nyeupe mbili (02) (tetroni) mikono mifupi zisizobana mikononi wala kiunoni, zinazokuenea vizuri na zenye uwezo wa kuchomekeea.
- ii. Suruali mbili (02) zenye rangi ya damu ya mzee na zisiwe za kubana (model). Kila suruali iwe na marinda mawili (02) na mifuko mitatu tu. Sampuli ya kitambaa imeambatanishwa kwenye barua hii.
- iii. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye gidamu (kamba) na kisigino kifupi.
- iv. Soksi ndefu nyeusi (jozi mbili).
- v. Mkanda mweusi wenye chuma kidogo kisicho na marembo yoyote.
- vi. Sare ya michezo (bukta nyeusi na tisheti yenye rangi ya damu ya mzee).

b. Wasichana.

- i. Shati nyeupe mbili (02) (tetroni) mikono mifupi zisizobana mikon wala kiuno, zinazokuenea sawasawa. Juba liwe lefu na litavaliwa juu ya shati yenye mikono mirefu na sketi ndefu.
- ii. Sketi mbili (02) zenye rangi ya damu ya mzee. Sketi iwe na marinda sita (06) na iwe ndefu. Sampuli ya kitambaa imeambatanishwa kwenye barua hii.
- iii. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye gidamu (kamba) na kisigino kifupi.
- iv. Soksi ndefu nyeupe (stocking) (jozi mbili).
- v. Sare ya michezo (bukta nyeusi na tisheti yenye rangi ya damu ya mzee)

2.1. Vifaa vya Taaluma

- i. Daftari kubwa kumi (10), ikiwezekana, zinunuliwe “Counter books”.
- ii. Mkebe wa mahesabu (Mathematical set).
- iii. Kalamu za kutosha na rula yenye urefu wa futi moja.

3.0. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Ni marufuku kwa wanafunzi:

- i. Kutumia madawa ya kulevyta kama vile Pombe, Cocaine, Heroine, Bangi, Kuber, n.k;
- ii. Kuvuta sigara au ugoro.
- iii. Kufuga nywele ndefu, kufuga ndevu au kucha
- iv. Kuvalaa bangiri, kupaka madawa kwenye nywele, kupaka dawa kwenye midomo.
- v. Kutofanya mitihani au majaribio yoyote (mitihani ya ndani, mock Form two, Form three na Form four).
- vi. Kukataa adhabu ya Mwalimu/Mlezi yeyote au Kiranja wa Shule/darasa
- vii. Kutoroka vipindi au kukwepa kazi za nje ya darasa kwa makusudi.
- viii. Kujibizana, kufokeana na Mwalimu au Mlezi au kuonyesha kiburi kwa Mwalimu/Mlezi
- ix. Kutoa lugha ya matusi kwa wanafunzi wenzake, viranja, Mwalimu au Mlezi yeyote.

Makosa yanayoweza kusababisha kufukuzwa Shule mara moja:

- i. Wizi
- ii. Uasharati, ubakaji na ushoga
- iii. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyta
- iv. Uvutaji bangi
- v. Makosa ya Jinai
- vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma
- vii. Kudharau Bendera ya Taifa
- viii. Kuoa au kuolewa
- ix. Kupata mimba au kusababisha mimba
- x. Kugoma au kuchochea mgomo
- xi. Kukataa adhabu ya Kiongozi/Mlezi au Mwalimu
- xii. Kupiga au kupigana.

3.1 Mambo Mengine Muhimu:

- **Form for Medical Examination:** Fomu hii imeambatanishwa ili ijazwe na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali na itarudishwa shulenii
- **Cheti cha Kuzaliwa:** Mwanafunzi aje na Nakala halisi (original) ya cheti cha kuzaliwa na kivuli cha cheti hicho. Atarudishiwa nakala halisi atakaporipoti kwa mara ya kwanza shulenii.

KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI BUZEBAZEBA.

FIDELIS P. BISAKARA

MKUU WA SHULE

HEADMASTER
BUZEBAZEBA SECONDARY SCHOOL
KIGOMA

FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

(To be completed by a Medical Officer in respect of all form one/Five Entrants)

Full Name

Age:

Sex:

Blood count (Red and White):

Stool Examination:

Urine analysis:

Syphilis test:

T.B. Test:

Ears:

Chest:

Spleen:

Abdomen:

ADDITIONAL INFORMATION e.g. Physical directs or impairment (s) infection

Chronic or Family diseases.

.....
.....
.....

I certify that the above is fit to pursue as stated above.

Signature:

Designation:

Date:

Station:

Note: Medical Office: At time of Examination please treat the Individual for Any ailments you note.

NB: This completed form should be sent to the school or brought when you come to school. No pupil may enroll without Certificate of physical fitness.